TANGAZO LA SERIKALI NA.100 la tarehe 24/2/2023

SHERIA YA MIPANGO MIJI,
(SURA YA 355)

# AMRI

*(Imetolewa chini ya kifungu cha 8(1) na 23(1))*

AMRI YA MIPANGO MIJI YA KURASIMISHA MAKAZI YASIYOPANGWA KATIKA ENEO LA MTANGANI YA MWAKA, 2023

Jina

1. Amri hii itajulikana kama Amri ya Mipango Miji ya Kurasimisha Makazi yasiyopangwa Eneo la Mtangani ya Mwaka, 2023.

Utangazaji wa eneo la upangaji Sura ya 355

2. Eneo lililobainishwa katika Jedwali la Amri hii linatangazwa kuwa eneo la upangaji (mpango wa urasimishaji) kwa madhumuni ya Sheria ya Mipango miji.

Mpango katika eneo la kwenye Jedwali

3. Mipango ya jumla na kina katika eneo la kwenye Jedwali itaandaliwa na kuhifadhiwa kwa Mkurugenzi wa Mipango Miji na Mkurugenzi wa Mji wa Mafinga.

______

JEDWALI

_______

*(Limeandaliwa chini ya aya ya 2)*

Eneo la upangaji lipo ndani ya mipaka ifuatayo:

"Unaanzia kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba HMQ 745 kwenye makutano ya barabara kuu ya Mafinga – Mgololo yenye majira - nukta 755191.367MS, 9080020.277KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Mashariki kwa umbali wa kilomita 1.00km hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba HMV 704 yenye majira - nukta 756178.916MS, 9080201.800KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Mashariki kwa umbali wa kilomita 0.32km hadi kwenye makutano na mkondo wa mto Mselefyuko kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba MTG 08 yenye majira - nukta 756496.142MS, 9080162.897KZ; baada ya hapo mpaka unafuata mkondo wa mto Mselefyuko kwa upande wa Kusini kwa umbali wa kilomita 1.00 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba MTG 07 yenye majira - nukta 756352.754MS, 9079485.862KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Mashariki kwa umbali wa kilomita 0.18 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba MTG 06 yenye majira - nukta 756272.347MS, 9079332.000KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini - Mashariki kwa umbali wa kilomita 0.24 hadi kwenye makutano ya barabara ya Magereza ya Isupilo kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba MTG 05 yenye majira - nukta 756397.723MS, 9079129.652KZ; baada ya hapo mpaka unafuata barabara hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba MTG 04, MTG 03 na MTG 02 zenye majira-nukta 756072.453MS, 9079065.315KZ, 755849.000MS, 9079037.412KZ, 755008.000MS, 9079050.000KZ; baada ya hapo mpaka unafuata barabara kwa umbali wa kilomita 0.16 hadi kwenye makutano ya barabara kuu ya Mafinga – Mgololo hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba MTG 01 yenye mjira - nukta 754913.000MS, 9079174.000KZ; baada ya hapo mpaka unafuata barabara ya Mafinga - Mgololo kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba HMQ 745 hadi ulipoanzia''.

Dodoma,
6th February, 2023

ANGELINE S. MABULA
*Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi*